# SIFA WANAZOTAKIWA MAKHALIFA KUWA NAZO NO.2

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

SIFA WANAZOTAKIWA MAKHALIFA KUWA NAZO No2

.kufikiri na kutafakari katika kuiongoza jamii .3

katika maelezo yaliyopita tulielezea sifa ya pili wanayotakiwa Mitume kuwa nayo, nayo ni uadilifu, tukiendelea na mada yetu katika kipengele hiki tutaelezea sifa ya tatu, nayo ni kutafakari katika kuiongoza jamii, miongoni mwa nyadhifa anazotakiwa kiongozi wa jamii ya Kiislamu, au hata isiyo ya kiislamu kuwa nazo ni kuwa yeye anatakiwa azingatie maslahi na manufaa ya watu wa jamii hiyo anayoiongoza, na yeye ndiye anayeweza kutoa amri ya kuwa watu wapigane vita, au wakubali suluhu,na katika hatua ya mwanzo, yeye ndiye mwenye hiyari na anayeweza kuitumia mali ya Baytul mali kutokana na maslahi ya jamii, basi wadhifa huo mkubwa ni lazima apewe mtu anayestahiki kuwa khalifa baada ya Mtume Muhammad -:((s.a.w.w), kama anavyosema Imamu Ali (a.s

ايها الناس ان أحق الناس بهذ الامر أقواهم عليه[1]

Enyi watu; mtu M-bora miongoni mwenu anayestahiki kupewa ukhalifa ni yule ambaye . -anaweza - kuiongoza jamii katika maadili ya kiislamu

Na ni jambo lililowazi kabisa kuwa baada ya Mtume Muhammad (s.a.w.w) Imamu Ali (a.s) ndiye aliyekuwa M-bora wao, - na elimu ya historia inathibitisha hayo - . kama tunavyosoma -: katika kitabu chake cha nahjulbalagha

و انه ليعلم أن محلى منها محلى القطب من الرحى[2]

Imamu Ali (a.s) anasema Yeye na ukhalifa ni vitu viwili visivyotengana, ni sawa na sehemu ya .kinu na mchi wake

ni sawa na position of pestle in the mill - .hii inaonyesha umuhimu wa nasabu yake Imamu - .Ali katika ukhalifa

Kwa hiyo Imamu Ali (a.s) alikuwa anaelewa kuwa cheo cha ukhalifa kwake Yeye ni jambo la)* .(lazima katika jamii ile ya kiislamu

.Mwanasiasa bora, ni yule awezae kutambua hila za maadui wake .4

Viongozi wa Kiislamu ni lazima wawe wajuzi katika kufahamu hila za maadui zao. kiasi ya kwamba waweze kupambanua baina hila zao na ukweli wao, kwa kufanya hivyo watakuwa wamewasaidia wafuasi wao kujua mbinu na hila za maadui wao. kama anavyoeleza Allah (s.w) .kuhusiana na ushindi watakaoshinda Waislamu katika vita, au maadui kushindwa

-: Mwenyeezi Mungu Mtukufu anasema

وَإِذَا جَاءهُمْ اَمْرٌ مِّنَ الاَمْنِ اَوِ الْخَوْفِ اَذَاعُواْ بِهِ وَلَوْ رَدُّوهُ إِلَي الرَّسُولِ وَإِلَي أُوْلِى الاَمْرِ مِنْهُمْ لَعَلِمَهُ الَّذِينَ يَسْتَنبِطُونَهُ مِنْهُمْ وَلَوْلاَ فَضْلُ اللهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ لاَتَّبَعْتُمُ الشَّيْطَانَ إِلاَّ قَلِيلاً[3]

Na linapo wafikia jambo lolote lilio khusu amani au la kitisho wao hulitangaza. Na lau kuwa wangeli lipeleka kwa Mtume na kwa wenye mamlaka kati yao, wale wanao chunguza wangeli lijua. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake mngeli mfuata .Shet'ani ila wachache wenu tu

Wanakatazwa hapa watu kutangaza mambo yaliyohusu siasa ya dola. Wasiyaseme ila yale * yaliyosemwa na hao wakubwa, kwani wao ndio wanaojua yepi yanafaa na yepi hayafai .kusemwa

baada ya Mtume Muhammad (s.a.w.w) kufariki, Imamu Ali (as) ndiye aliyekuwa mjuzi zaidi .kuliko wengine ambaye alizielewa mbinu za maadui wa Kiislamu nje na ndani ya nchi

kimya cha Ali (amani iwe juu yake) cha muda wa miaka 25 baada ya mtume (amani iwe juu yake), ukiongezea na ile miaka 5 ambayo aliitumia akiwa ni kama khalifa, ni vitu viwili vilivyo .weza kuzuia utokeaji wa machafuko

-:Imamu Ali (a.s) anasema

فأما الناكثون فقد قاتلت * وأما القاسطون فقد جاهدت * وأما المارقة فقد دوخت"[4]“

Katika vita vya jamal nilipigana nao wale waliopinga ujumbe wa Mwenyeezi Mungu, na nilipigana jihadi katika vita safayn kwa wale waliopigania haki, na katika vita vya Nahriwan . - nikawachanganya wale walioritadi dini - wale waliotoka nje ya dini

[1] Nahjulbalagha, خ 173, Nahjulbalagha, Feydh, خ 172

[2] Nahjulbalagha خ 3

[3] Surat Nisaa Aya ya 83

[4] Nahjulbalagha, sabhy. خ. 192. Nahjulbalagha Feydh. خ 234

MWISHO